

HAZARD HISTORIES

Utangulizi: Kutegemea na jiografia ya eneo katika jamii, hatari fulani zinaweza kutokea zaidi kuliko zingine. Kwa mfano, watu wanaoishi katika kisiwa cha kitropiki hawahitaji kujiandaa na dhoruba ya theluji ya Artiki, lakini wanaweza kulazimika kujiandaa na hatari ya upepo wa sunami. Ni muhimu kuelewa hatari zako za maafa, ili uchukue hatua stahiki ya kujiandaa na hatari ili kusaidia kuzuia athari zake kugeuka kuwa maafa. Kutokana na hatari fulani huenda zikaitokeza mara kwa mara ndani ya jamii, manajamii wanaweza kuwa na maarifa asilia juu ya namna ya kujiandaa. Maarifa asilia pamoja na mbinu za utayari ni muhimu kuzishika na kuzifanyia mazoezi ili kusaidia katika kukabili hatari ya maafa asilia.

Shughuli za Kupunguza Hatari Ya Maafa

Muda

Dakika 30 - Saa 1

Ugumu

Rahisi

Rasilimali

Penseli, karatasi

● Hatua ya 1

- Fikiri kuhusu jamii yako. Ni hatari zipi hutokeza mara kwa mara unapoishi?

● Hatua ya 2

- Zungumza na wazee katika jamii yako ili kujifunza zaidi kuhusu hatari zilizokabili eneo lenu. Kwa ridhaa yao, unaweza kuandika maelezo au kurekodi simulizi yao ili kupata mwongozo wao mzuri. Jamii yako inafanya nini ili kujiandaa? Kuna hatari yoyote ile iliyobadilika kuwa maafa, kama ndiyo jamii yako ilifanya nini kukabiliana wakati wa tukio na kurejesha amani baadaye? Wazee wamewahi kukumbana na hatari yeyote katika jamii wakati wa ukuaji wao? Hatari zilizokumba jamii hapo nyuma zina utofauti na hatari zinazotokea wakati wa sasa? Kuwa mdadisi kuhusu uzoefu wao ili kujifunza zaidi kuhusu historia ya jamii yako.

● Hatua ya 3

- Fikiri kuhusu namna ambayo unaweza kuwashirikisha wenzako au kizazi cha vijana ili kuhakikisha jamii yako inaendelea kujijenga juu ya tabia asilia ya utayari.

